# Muhtasari wa Wachangiaji wa Jamii

## Sisi ni nani

Tume ya Wakimbizi Wanawake (WRC) inaboresha maisha na kulinda haki za wanawake, watoto na vijana ambao wametoroka makwao kufuatia mizozo na ghasia. Tunasafiri kwenda katika makazi ya wakimbizi na kuzungumza nao ili kufahamu wanachohitaji. Tunazungumza pia na mashirika ya UN na mashirika ya kimataifa na ya nchini. Kisha tunayapa maoni mashirika ya kimataifa na kitaifa kuhusu mambo ya kufanywa ili kuboresha maisha ya wakimbizi na wengine waliotoroka makwao kufuatia mizozo na majanga.

## Mambo tuliyofanya nchini Kenya

WRC ina mradi ambao unachunguza dhuluma za kingono dhidi ya wakimbizi wa kutoka Kongo, Somalia wa Sudani Kusini ambao ni wanaume, wavulana na wanawake aliobadilisha jinsia ambao wanaishi mjini Nairobi na Mombasa. Dhuluma za kingono zinaweza kujumuisha kujeruhiwa sehemu za siri au kulazimishwa kufanya ngono na mtu mwingine. Zinaweza pia kujumuisha kulazimishwa kumtazama mtu mwingine akidhalilishwa kingono, au kununua ngono kutoka kwa mtoto. Watu wanaowadhulumu wengine kingono (wahalifu) mara nyingi huwa wanaume, lakini wanawake pia wanaweza kusababisha dhuluma za kingono. Mwezi Aprili na Mei 2019, mtafiti wa WRC alisafiri kwenda Nairobi na Mombasa kupata maelezo zaidi kuhusu maswala haya. WRC ilifanya vikao vya vikundi 24 maalum vyenye wakimbizi 149 na kuwahoji wafanyakazi wa kutoa misaada na watoa huduma 40. UNHCR (shirika la wakimbizi la UN) na HIAS, na pia viongozi wa jamii na wakalimani, walitusaidia katika utafiti wetu.

## Mambo tuliyogundua

Una haki ya kujua matokeo ya uchunguzi huu. WRC iligundua kuwa:

- Wakimbizi wengi ambao ni wanaume, wasichana na wavulana walidhulumiwa kingono kabla, wakati wa, na baada ya kukimbilia nchini Kenya.
- Dhuluma za kingono dhidi ya wanaume na wavulana, na pia dhuluma za kingono dhidi ya wanawake na wasichana, zinaonekana kutokea mara nyingu katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Sudani Kusini. Watu wengi walidhulumiwa kingono wakati wa shambulio la nyumbani na waliposimamishwa kiholela, walipokuwa wameshikwa mateka na kuwekwa kizuizini, na katika mipaka na vituo vya ukaguzi.
- Nchini Somalia, baadhi ya wanaume na wavulana walidhulumiwa kingono na wafamilia na wanajamii, wanachama wa koo zingine, na vikosi vyenye silaha, lakini haijulikani dhuluma za kingono hutokea kwa kiasi gani.
- Wanaume wengi mashoga na wanawake waliobadilisha jinsia walisema walidhulumiwa kingono katika nchi zao na nchini Kenya, dhuluma ambazo zilitekelezwa na wafamilia na wanajumuiya, maafisa wa polisi, na wengine.
- Mjini Mombasa, unyanyasaji wa kingono dhidi ya wavulana na vijana wakimbizi wa kiume unaonekana kutokea mara nyingi.
- Mjini Nairobi na Mombasa, wakimbizi walio katika hatari kubwa ya kudhulumiwa kingono ni pamoja na wanaume na wavulana mashoga, watu waliobadilisha jinsia, wavulana na vijana wakiume wasioandamana na watu wengine, wakimbizi wanaouza ngono, na wafungwa.
- Waathiriwa wa dhuluma za kingono mara nyingi huwa na mahitaji mengi ya kimatibabu, kisaikolojia na kijamii. Huduma chache zinapatikana jijini Nairobi na Mombasa za kuwasaidia wanawake na wanaume wakimbizi, ikijumuisha wanaume mashoga na wanawake waliobadilisha jinsia. Wakisaidiwa, watu wengi waliodhulumiwa kingono wanaweza kupona na kuishi maisha kamili na ya kawaida.
- Kuna vizuizi ambavyo vinawazuia wakimbizi kupata huduma. Kwa mfano, baadhi ya wakimbizi hawana maelezo ya kutosha kuhusu huduma zinazopatikana. Huenda hawajui mahali anapoweza kupata usaidizi mwanaume, mvulana, au mtu aliyebadilisha jinsia ambaye amedhulumiwa kingono. Watoa huduma za afya, wafanyikazi wa jamii, na wengine huenda wasijue kuwa wanaume na wavulana wanaweza kulengwa kwa aina hii ya dhuluma, au wanaweza kuwakoea heshima waathiriwa.

## Je, ingekuwaje ikiwa hili lilinifanyikia mimi au mtu ninayemjua?

Dhuluma za kingono KAMWE sio kosa la mhasiriwa. Ni kosa la mtekelezaji. Mtu yeyote anaweza kulengwa katika dhuluma za kingono. Dhuluma za kingono zina athari za kimatibabu na kisaikolojia ambazo zinaweza kutibiwa au kudhibitiwa.

Ikiwa wewe au mtu unayemjua amedhulumiwa kingono na anahitaji usaidizi wa kimatibabu na/au afya ya akili:

- Piga simu kwa polisi kwa nambari maalum ikiwa uko katika hatari ya dharura: 999 au 112.
- Piga simu kwenye nambari maalum ya kitaifa ya masuala ya dhuluma za kingono na kijinsia: 1195. Nambari hii hailipishwi na inafanya kazi saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki.
- Mjini Nairobi, piga simu kwenye nambari maalum ya MSF ya masuala ya dhuluma za kingono na kijinsia: 0711 400 506.
- Nenda kwenye hospitali iliyo karibu zaidi upate huduma ya haraka ya kimatibabu au kisaikolojia.
- Nenda kwenye Nairobi Women's Hospital (mjini Nairobi na Mombasa) Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta, Hospitali ya Mama Lucy Kibaki, au kliniki ya MSF mtaani Mathare. Hospitali hizi zina huduma maalum za waathiriwa wa dhuluma kingono na kijinsia. Hospitali hizi hufunguliwa saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki.

## Hatua zinazofuata ni gani?

Tume ya Wakimbizi Wanawake imechapisha ripoti kamili kuhusu matokeo na maoni kutoka kwa utafiti huu, "Tuna Mioyo Iliyovunjika": Dhuluma za kingono dhidi ya Wakimbizi mjini Nairobi na Mombasa, Kenya. Ripoti kamili inapatikana kwa Kiingereza, na muhtasari mkuu unapatikana kwa Kiingereza na Kiswahili kwenye https://www.womensrefugeecommission.org/svproject.

WRC inashirikiana na HIAS kufanya jaribio la mradi wa kusaidia ushirikishaji jamii za LGBTIQ wa Kenya na wakimbizi.

## Maelezo ya mawasiliano

Dale Buscher,
Makamu wa Rais, Mipango
Tume ya Wakimbizi Wanawake
Simu: +1 212 551 3115
daleb@wrcommission.org

Dkt. Sarah Chynoweth
Mkurugenzi/Mshauri wa Masuala ya Dhuluma za Kingono wa
Tume ya Wakimbizi Wanawake
Simu: +1 212 551 3115
svproject@wrcommission.org

Dr. Vincent Were
Kenya Medical Research Institute
Sanduku la Posta, 1578-40101
Kisumu, Kenya
Simu: +254 721 876 573
vwere@kemricdc.org

Oktoba 2019